



SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR  
WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO  
TAARIFA KWA UMMA

TAHADHARI YA SERIKALI JUU YA ANUAI MPYA YA KIRUSI  
CHA SARS-COV2 Tarehe: 29 Novemba, 2021

Ndugu Wananchi,

Serikali imekuwa ikiendelea kupambana na mripuko wa UVIKO-19 ambao umekuwa ukiendelea katika maeneo tofauti ya nchi yetu. licha ya kuonekana kupunguwa kasi, bado visa vya wagonjwa na vifo vimekuwa vikitolewa taarifa katika eneo letu. Hata hivyo, siku ya Ijumaa, shirika la Afya Duniani (WHO) limetoa taarifa juu ya uwepo wa anuai mpya ya SARS-COV-2 ambayo mwanzoni ilijulikana kwa jina B.1.1.529 na kwa sasa kinaitwa **Omicron**, kirusi hiki kinaonekana kuongezeka katika maeneo na majimbo mengi ya Afrika Kusini. Aidha, taarifa zinaonesha kwamba kirusi hiki pia kimetolewa taarifa katika nchi za Botswana, Belgium, China na Israel.

Ndugu Wananchi,

Kkirusi hiki inasemekana kina uwezo mkubwa wa kuambukiza zaidi kwa watu lakini bado njia za kujikinga ni zile zile. Hivyo serikali inatoa wito kwa Wananchi na makundi yote katika jamii kuendelea kuchukua tahadhari na kutekeleza afua zote ambazo Wataalamu wa **Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto** wamekuwa wakiwasihii Watu kuchukua ikiwemo;

1. Uvaaji wa Barakoa
2. Kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka au kutumia vitakasa mikono
3. Kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima pamoja na kukaa katika sehemu zenye mzunguko wa hewa ya kutosha.
4. Wananchi wote ambao bado hawajachanja, wafanye hivyo katika vituo vyetu vilivyotangazwa na kupitia huduma zetu za mkoba zinazoendelea nchi nzima

Ndugu Wananchi,

Mwisho na sio kwa umuhimu, natoa wito kwa watumishi wote wa Afya katika maeneo ya **Bandari, Viwanjwa vya ndege na katika vituo vyetu vya afya** ngazi zote kuendelea kufuatilia wateja wote wanaotumia maeneo tajwa hapo juu na pale wanapopata mshukiwa wa UVIKO-19, wachukuwe sampuli na kuiwasilisha kwa ajili ya kuipima kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Wakati huohuo, napenda kuwashukuru mashirika na wadau mbalimbali ambao wamekuwa bega kwa bega na serikali katika kukabiliana na UVIKO-19 nchini, serikali inawahakikishia kwamba bado itaendelea kutoa ushirikiano kila mara itakapohitajika.

Jikinge na umkinge mwenzio, UVIKO-19 inazuilika.

Mhe Nassor Ahmed Mazrui

Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto  
**Zanzibar.**